**HOTUBA YA MKUU WA WILAYA YA MPWAPWA KWENYE MAADHIMISHO YA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA WILAYA YA MPWAPWA TAREHE 16/06/2018.**

Waheshimiwa Madiwani

Ndugu Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Mpwapwa

Ndugu Viongozi wa Serikali na Vyama vya Siasa

Ndugu Viongozi wa Dini, Taasisi na Mashirika Mbalimbali

Ndugu Wakuu wa Idara

Watoto wote

Ndugu wageni waalikwa, Mabibi na mabwana

Ndugu Wananchi,

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha Siku hii ya leo.

Pia napenda kuwapa hongera wale waliojaliwa kujinyima na kufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani naomba Mola awaongezee thawabu.

Aidha, napenda kuwashukuru sana na kuwapongeza ninyi nyote mlioitikia wito wa kufika hapa siku hii ya leo, tunawapongeza jinsi ambavyo mmeandaa Maadhimisho ya siku ya Mtoto katika Wilaya yetu hii ya Mpwapwa, mlivyoweza kushiriki nyinyi pamoja na watoto wetu, hivyo nawapongezeni sana.

Shukrani za kipekee ziwaendee Shirika lisilo la Kiserikali la Compassion kupitia Makanisa ya TAG, KKKT, Mt. Paul, EAGT Sayuni na Kanisa la Watakatifu wote na Shirika la Jukwaa la Utu wa Mtoto (Children's Dignity Forum). Aidha, napenda kutoa shukrani kwa Benki za NMB, CRDB Mpwapwa na Wafanyabiashara kwa michango yao na kuwezesha kufanikisha maadhimisho ya siku ya leo.

**Ndugu Wananchi,**

Nimefurahi pia kupata nafasi hii ya kuwa Mgeni Rasmi katika maadhimisho haya ya siku ya Mtoto wa Afrika yanayoadhimishwa kiwilaya hapa leo Kata ya Lupeta. Lakini pia nimefurahi kuona maonyesho, shughuli za vipaji mbali mbali vya watoto zikiwemo nyimbo, maigizo Sarakasi na Mashairi. Nawapongeza sana kwa wale watoto walioonesha vipaji vyao na natoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya

kuendelea kuvilea, kuviendeleza na kuvikuza vipaji hivi ili baadae watoto pamoja na Taifa letu liweze kunufaika na vipaji hivi. Aidha, nimesikia Risala ya watoto ambayo imejumuisha haki za kimsingi za watoto ambayo imebainisha wazi changamoto wanazopitia watoto wetu zenye kukatisha ndoto zao lakini pia yenye kutoa majukumu ya kila mdau yaani wazazi/walezi, familia, taasisi za dini, asasi za kiraia na jamii kwa ujumla katika kukabiliana na changamoto hizo.

**Ndugu wananchi,**

Baada ya kusema haya, ningependa kwa ufupi kueleza hasa nini madhumuni ya kuadhimisha siku hii ya Mtoto wa Afrika tarehe 16 Juni kila mwaka. Siku hii huadhimishwa na nchi huru za bara la Afrika, Tanzania ikiwa ni mojawapo. Madhumuni ya kuadhimisha siku hii, kwanza ni kumbukumbu ya Mateso na Kunyanyaswa kwa watoto wa kitongoji cha Soweto huko Afrika ya kusini wakati wa Utawala wa Kikaburu, siku ambayo watoto wa Soweto waliandamana kupinga Sheria mpya ya Makaburu katika kufundisha shule zote kwa lugha ya kigeni. Siku hiyo watoto waliandamana kwa nia ya kusikilizwa shida zao. Matokeo yake Askari wa Makaburu waliamriwa kuwatawanya kwa nguvu. Katika kufanya hivyo walifyatua risasi na kuwauwa watoto wengi. Jambo ambalo ni ukatili kwa watoto. Lakini pia ni fursa kwetu kukaa chini na kutafakari juu ya hali ya ulinzi pamoja na ustawi wa watoto wetu kwani watoto ni nguzo imara ya jamii yoyote iliyoendelea.

Kila Mwaka maadhimisho haya huambatana na kauli mbiu zenye lengo la kuunganisha nguvu za pamoja katika kukuza ustawi wa mtoto. Kauli mbiu ya mwaka huu kwa bara la Afrika inasema "***TUSIMWACHE MTOTO NYUMA***" na kwa kuwa nchi yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dr John Pombe Magufuli imedhamiria kuingia kwenye uchumi wa Viwanda, Kauli mbiu yetu kwa Tanzania inasema **"KUELEKEA UCHUMI WA VIWANDA; TUSIMUACHE MTOTO NYUMA"**

**Ndugu wananchi,**

Kimsingi Sera ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania ya Mwaka 2008 na Sheria ya mtoto namba 21/2009 zimetungwa na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano na kusainiwa na Mheshimiwa Rais. Lengo hasa la utungwaji wa Sera na sheria hizi ni kuwezesha ulinzi wa kijamii na kisheria kwa watoto na kusaidia

mifumo rasmi yenye kutekeleza na kusimamia haki za mtoto kuweza kutoa haki na kutekeleza sheria ipasavyo ikiwemo haki ya kuendelezwa.

**Ndugu wananchi,**

Awamu ya tano ya mfumo wa Utawala nchini imekuwa na msisitizo mkubwa wa kujenga uchumi wa kati ambao msingi wake ni maendeleo ya viwanda. Msisitizo huu umelenga katika kuanzisha viwanda vidogo vya Kati na vikubwa vya uzalishaji wa bidhaa katika ubora unaotakiwa.

Viwanda vingi havina budi vitokane na kazi za mikono za kiufundi kama vile ususi, uchoraji, uashi, uchomeaji na uyeyushaji wa malighafi za asili ya chuma. Pia usindikaji wa malighafi za kilimo na ufugaji kama vile matunda, mboga mboga, nafaka, maziwa, nyama, na mayai.

Wataalamu wa elimu wamekuwa na mijadala mbalimbali kuhusu ni kwa kiwango gani mifumo yetu ya elimu rasmi inavyoweza kuchangia malengo hayo. Wamekuwa wakiangalia pia uwezo wa wasomi wetu wanaozalishwa na taasisi zetu za elimu ni kwa kiwango gani wana uwezo wa kufanikisha kufikiwa kwa Tanzania ya Viwanda.

**Ndugu wananchi,**

Pia wataalamu wa saikolojia ya Jamii nao wameeendelea kushauri ni kwa kiwango gani malezi na makuzi yetu yanahitajika kujikita katika kubaini na kuviendeleza vipaji vya ubunifu lakini pia kujenga uthubutu kwa vijana wetu kuanzisha viwanda vidogo na kujihusisha na uzalishaji

Makundi yote hayo yana lengo moja la kuhakikisha yanatoa mchango wao katika kukuza uchumi na hali za maisha ya wananchi kiuchumi, kimaadili, kisiasa na kiutamaduni.

## Uendelezwaji wa Watoto

**Ndugu wananchi**

Zipo sababu za kibaiolojia, kimazingira na mifumo ya tamaduni za kijamii inavyoathiri maendeleo ya watoto na vijana kufikia kujiamini na kuthubutu kuchangia maendeleo ya kaya na taifa kwa ujumla.

**Vipindi vya Makuzi na Malezi ili Tupate Vijana Wenye Vipaji**

**Malezi Miaka Mitatu hadi Sita**

Kipindi hiki ni muhimu kwa wazazi, walezi kuwapa watoto fursa za kucheza michezo mbalimbali. Jukumu la wazazi linapaswa kuwa ni kuhakikisha usalama wa kimazingira na kuwezesha katika vifaa vya kuchezea. Katika kipindi hiki watoto wanahitaji kucheza ikiwa ni pamoja na kucheza na marafiki, ni vyema wazazi wawaruhusu pasipo kuhofu kuchafuka kwani huwajengea afya bora ya mwili na akili.

Watoto wana kawaida ya kutengeneza ratiba zao za michezo ambazo wakati mwingine ni tofauti kabisa na ufikiri wa watu wazima. Hivyo, wanapojitungia michezo yao, watu wazima wawape uhuru huo wa kucheza ikiwa ni pamoja na uwepo wa uangalizi wa wazazi au watu wazima ili kuhakikisha michezo iliyo hatari na yenye kuepuka maadili inaepukwa.

Watoto wanapocheza katika mazingira ya shule au nyumbani wanakuza fikra na ndoto zao za maisha ya baadae. Ndoto hizo zinapaswa kukuzwa kwani huwawezesha kujenga picha ya ni kina nani wanataka wawe baadae katika jamii yao na Dunia kwa ujumla.

Familia nyingi na jamii kwa ujumla zimekuwa haziwekezi katika vifaa na viwanja vya michezo ya watoto. Kweli ni gharama lakini hatuna budi kufanya hivyo.

**Ndugu wananchi,**

**Malezi katika kipindi cha Miaka 6 hadi 11.**

Kipindi hiki watoto wengi wamekuwa tayari wapo shuleni. Inafahamika kuwa shule ni wakala Mkubwa wa mabadiliko. Kuwepo kwa Sera ya elimu bure kumeongeza idadi ya watoto wanaoandikishwa katika ngazi ya elimu ya Msingi.

Wajibu wa jamii uwe kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa, lakini pia jamii isisahau kuwezesha watoto hao katika mahitaji mengine muhimu shuleni kwa kushirikiana na uongozi wa shule na pia kuhakikishiwa ndoto zao za elimu hazikatishwi kwa sababu yoyote ikiwamo ndoa na mimba za utotoni.

Shuleni wanafunzi wapewe fursa ya kushiriki michezo mbali mbali na kazi za sanaa na ubunifu. Tumeshuhudia idadi kubwa ya vijana wakitaka kushiriki katika

shughuli za sanaa na uigizaji, uchekeshaji, uongozi wa sherehe na matukio, muziki na urembo.

Ni vyema pia mkazo ukawekwa katika shughuli zinazohusisha ufugaji, kilimo na elimu ya ujasiriamali. Hasa katika kipindi hiki ambacho Wilaya yetu imeweka mkazo katika kuanzisha zao la Korosho ambalo litakuwa mkombozi mkubwa kwa Uchumi wa Wilaya yetu ya Mpwapwa, ni muhimu kuendelea kuhakikisha wanajifunza kwa vitendo kupitia mashamba mfano ya shule juu ya uendelezaji wa zao hili la Korosho.

Kwa kusema haya, Jamii inaposisitiza uanzishaji wa viwanda mbalimbali ni vema sasa ikawekeza kuanzia kwa watoto wetu ili kupata suluhu ya Kudumu na isiyo ya kipindi kifupi. Msisitizo mkubwa uwekwe katika elimu ya Sayansi na ufundi, sambamba na kutengwa kwa maeneo ya viwanja vya Uwekezaji kwa vijana.

**Ndugu wananchi,**

Mtoto ametafsiriwa katika kifungu cha 4(1) cha sheria ya mtoto kuwa ni mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane (18). Sheria imeainisha haki za mtoto ikiwa na maana stahili muhimu za mtoto kumuwezesha kufurahia, na kuendelea kwake kuishi. Zaidi, sheria imeainisha wajibu wa mtoto kwa familia, jamii na nchi yake.

**Ndugu wananchi,**

Kuna haki mbalimbali zinazomuhusu mtoto ikiwemo haki ya kuishi, haki ya kupata jina, haki ya urithi, haki ya kutobaguliwa, haki ya kuendelezwa, haki ya kutoa mawazo katika masuala yanayomgusa maslahi yake na haki ya ulinzi.

**Ndugu wananchi,**

Kifungu cha 8(1)-(2) kinatamka kuwa ni wajibu wa mzazi au mlezi anayeishi na mtoto kuweza kumtunza mtoto kwa kumpatia haki pamoja na mahitaji kama Chakula, Malezi ikiwa ni pamoja na makazi, matibabu na kupatiwa chanjo, elimu, uhuru, haki ya kucheza, kustarehe na kupumzika.

**Ndugu wananchi,**

Kifungu cha 21 na 27 ndio vyenye kutoa wajibu wa kimalezi kwa waangalizi wa watoto na mameneja wa Taasisi zinazolea watoto kama Compassion na makao ya watoto kwa kuainisha majukumu yafuatayo:- kuhakikisha maendeleo ya

mtoto yanafikiwa wakiwa chini yao kama kupata elimu na kuangaliwa vyema katika upande wa afya, kuwasiliana na wazazi juu ya maendeleo ya mtoto na Ulinzi wa mtoto kwa kipindi chote wawapo katika kituo.

**Ndugu wananchi,**

Sheria imeweka wajibu kwa jamii kwa kumtaka mwanajamii mwenye taarifa au ushahidi kuhusiana na mtoto ambaye haki zake zinakiukwa na mzazi, mlezi au ndugu au mtu yeyote kutoa taarifa kwenye Serikali za mitaa, vyombo vya dola au kupiga Simu namba 116 inayohusu huduma kwa mtoto Tanzania, huduma hii haina malipo yoyote. Wazazi tushirikiane katika kutoa taarifa kamili na sahihi kwa wale wote ambao wanawafanyia watoto vitendo viovu vikiwemo ubakaji na ulawiti ili Serikali iweze kuwachukulia hatua Kali za Kisheria kwa watakaobainika.

**Ndugu wananchi,**

Serikali za Mitaaa zina wajibu wa kulinda na kutetea maslahi ya mtoto katika eneo husika kupitia Afisa Ustawi wa Jamii. Serikali za Mitaa zitashirikiana na jeshi la Polisi katika kuwatafuta wazazi, walezi, na ndugu wa watoto waliotelekezwa kwa nia ya kuwapatia watoto malezi yaliyojengwa katika misingi bora.

**Ndugu wananchi,**

Wazazi na jamii wanalo jukumu la kuwalinda watoto kwa kuwazuia kushiriki kwenye maeneo ambayo yanaweza kusababisha vitendo viovu kufanyika ikiwemo vibanda vya kuonyesha Sinema, kufuatilia zawadi zinazotolewa kwa watoto kwa watu wasiofahamika na wazazi na walezi wa watoto, kuweka utaratibu mzuri na salama wa watoto kwenda na kurudi shule kwa maeneo au vijiji ambavyo shule zipo mbali na makazi ya wananchi ili kuwalinda watoto na watu wabaya wanaotumia umbali huo kuwatendea uovu watoto.

**Ndugu wananchi,**

Pia wazazi, Taasisi na jamii kwa ujmla wake ninawaomba kuendelea kuitikia wito wa Serikali na kila inapowezekana kujenga mabweni katika shule zetu za Sekondari ili kuwasaidia ulinzi kwa mtoto. Watoto walindwe ili waweze kutimiza ndoto zao na kufikia malengo yao. Wazazi tukumbuke kuwa toka miaka ya zamani mtoto ni wa wote hivyo ni jukumu letu kuendelea kumlinda kwa gharama zozote kwani **"Mtoto wa Mwenzio ni Mwanao Pia"**

**Ndugu wananchi,**

Iwapo Mamlaka ya Serikali za Mitaa haitafanikiwa katika kupata wazazi wa mtoto basi itaelekeza suala hilo kwa Afisa Ustawi wa Jamii. Afisa Ustawi wa Jamii na Polisi ni lazima wafanye Uchunguzi ndani ya eneo la Mamlaka ya Serikali za Mitaa juu ya ukiukwaji wa haki za mtoto.

**Ndugu wananchi,**

Kutokana na Changamoto zilizoainishwa kwenye Risala ya Watoto nitoe mwito kwa Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na wadau wengine wanaohudumia watoto kuweza kuwajengea Miundombinu rafiki kwa watoto ili kuweza kuibua vipaji mbalimbali walivyonavyo ikiwemo kutenga Maeneo ya Michezo, Kuandaa matamasha ya Maonyesho ya kuibua vipaji, na Alama za Barabarani hasa maeneo ya Shule. Aidha, Halmashauri isimamie sheria za majengo kuhakikisha yanayotumiwa na Jamii yawe na miundombinu rafiki kwa watoto na watu wenye ulemavu ili waweze kupata huduma kwa urahisi zaidi.

**Ndugu wananchi,**

Mwisho natoa ushauri kwa wadau wote wazazi/walezi, jamii, Taasisi za dini, Asasi za kiraia, Serikali za Mitaa na vyombo vya dola kushirikiana kwa karibu, kwa pamoja tutaweza kutekeleza kauli mbiu ya **KUELEKEA UCHUMI WA VIWANDA, TUSIMUACHE MTOTO NYUMA.**

**Mungu Wabariki Watoto Wote**

**Mungu Ibariki Mpwapwa**

**Mungu Ibariki Tanzania**

**Ahsanteni Sana kwa Kunisikiliza.**